


Karibu:



Serikali ya Kaunti ya Kitui

S.L.P. 460-90200, Kitui

Wizara ya Afya na Usafi

Hati ya Huduma ya Afya kwa Wagonjwa

Haki Zako

Kupokea huduma ya afya pamoja na matibabu ya dharura kwa wakati unaofaa bila kubaguliwa.

Kuhudumiwa kwa usawa bila kujali hadhi yako, ikiwemo Jinsia, Ulemavu, Umri, Hali ya Afya, Dini au uanachama wa kikundi cha walio wachache au cha watu wenye mahitaji maalumu.

Kupokea huduma bora zaidi ya afya iwezekanavyo ambayo haikuweki katika madhara yasihitajika; na kuhudumiwa na wataalamu wa afya waliohitimu, wanaotambulika na waliodhinishwa na wanaovalia sare rasmi.

Kuhudumiwa kwa adabu, huruma na heshima.

Kuwa na uhuru kutokana na mteso, ukatili, unyama na kuhujumiwa unapoendelea kupata matibabu katika kituo cha afya.

Kuhudumiwa kwa namna ambayo inaheshimu usiri wako na haki yako ya kudumisha usiri.

Kuwa na haki ya kuheshimiwa kimwili na kuhakikishiwa usalama wa utu wako unapoendelea kupata matibabu katika kituo cha afya.

Kupatiwa habari kamili, sahihi na inayoleweka na kwa wakati ufaao kuhusu afya yako na huduma za afya, kanuni na itifaki zake.

Kuhusishwa na kufahamishwa kuhusu maamuzi yakueleweka yaliyofanywa kuhusu afya yako na ikiwemo uchaguzi au haki ya kutafuta maoni ya muhudumu mwengine wa afya.

Kupokea huduma zaidi, kuhamishwa katika hospitali nyingine na mashauri yanayohitajika kwa utunzi wa afya yako.

Kukataa kupokea matibabu.

Kupokea habari wazi na zinazoleweka kuhusu huduma zinazotolewa bila malipo na gharama za huduma zinazotolewa bila malipo katika kituo cha afya.

Kuwa na mazingira safi na salama katika kituo cha afya.

Kutoa pongezi, maoni na malalamishi kuhusu huduma uliyopokea bila uwoga. Tunaahidi kwamba tutawasilisha malalamishi yako kwa wakati ufaao na kupitia kwa mchakato huru kwa manufaa yako na mtu mwengine yeyote anayehusika katika jambo hilo.

Wajibu Wako

Kufuata na kutii sera, kanuni na taratibu za kituo cha afya na kujaza fomu zozote kama inavyotakikana.

Kufuata mfumo wa huduma kwa yule aliyetangulia kuhudumiwa kwanza bila kujali hadhi yako ya kijamii, kisiasa au hadhi nyingineyo ila tu pale ambapo hali yako ni ya dharura na inahitaji kuhudumiwa kwa haraka.

Kuwaheshimu na kuwathamini wataalamu wa afya na wengine waliodhinishwa na wateja wengine.

Kuwapa wataalamu wa afya habari sahihi kuhusu afya yako na kuuliza maswali na kupata ufanuzi wa mambo usiyoyaelewa.

Kufuata matibabu yaliyoagizwa, hatua za urekebishaji na huduma fuatilizi za matibabu.

Kutia sahihi kwa ajili ya maamuzi yako ya kukataa kupokea matibabu yaliyopendekezwa na kituo hicho cha afya.

Kulipia tu yale malipo yaliyoidhinishwa kwa ajili ya huduma zinazohitaji malipo na kupata risti rasmi za malipo hayo; na kuwalishwa wasimamizi kama kuna hitilafu zozote.

Saa za Kutoa Huduma

Jumatatu hadi Ijumaa	Kuanzia.....	hadi
Jumamosi	Kuanzia.....	hadi
Jumapili	Kuanzia.....	hadi
Sikukuu za Umma	Kuanzia.....	hadi

Namba za Mawasiliano

Jina la Kituo cha Afya
Baruapepe
Nambari za Simu za Dharura
Nambari za Simu za Kutolea Maoni



Tusaidie ili tukusaidie!

Toa mapendekozu kuhusu jinsi tunavyoweza kukuhudumia vyema na jinsi unavyoweza kutusaidia kukuhudumia vyema zaidi. Unaweza kuwasilisha malalamishi kuhusu huduma ulizopata. Tunaahidi kulishughulikia swala hilo na kukupa majibu.

Tafadhali uisome hati yote kama ilivyotolewa katika vijitabu katika maeneo yetu ya kusubiri.

Ili kuimarisha utendaji kazi katika kituo hiki, hati hii itarekebishwa mara kwa mara baada ya majadiliano na umma na wadau.